**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO**

# MWONGOZO WA KITAIFA WA USIMAMIZI WA UNUNUZI WA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO KWA WASINDIKAJI

## 1.0 UTANGULIZI NA USULI

Sekta ya nafaka na mazao mchanganyiko ina mchango mkubwa katika usalama wa chakula, ajira na ukuaji wa uchumi wa Taifa. Katika kuimarisha biashara ya mazao, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) imeendelea kurasimisha biashara ya nafaka na mazao mchanagnyiko kwa mifumo mbali mbali ukiwemo Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na Minada ya Kidijitali ambapo inashirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) kwa lengo la kuongeza uwazi wa bei, ushindani wa haki, mapato ya wakulima pamoja na mapato ya Serikali.

Pamoja na mafanikio hayo, Serikali imeendelea kuweka mkazo katika kuongeza usindikaji wa mazao nchini ili kupunguza utegemezi wa kuuza mazao ghafi na kuongeza thamani ya bidhaa zinazouzwa ndani na nje ya nchi. Mathalani, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inalenga kujenga uchumi wa viwanda wenye ajira zenye staha na ushindani wa bidhaa zilizoongezwa thamani na kufikia uchumi wa takribani Dola za Marekani trilioni moja (1) ifikapo mwaka 2050. Aidha, Mpango Mkakati wa Mageuzi ya Kilimo (Agricultural Master Plan 2050) unalenga kuongeza thamani ya sekta ya uchakataji kwa mazao ya kilimo (agri-processing) kufikia Dola za Marekani bilioni tatu (3) ifikapo mwaka 2050, huku Agenda 10/30 ikisisitiza kuongeza usindikaji wa mazao na mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani.

Kutokana na mwelekeo huo, kuna umuhimu wa kuweka utaratibu maalum utakaowezesha wasindikaji wa ndani kupata malighafi kupitia mfumo rasmi wa biashara ya mazao huku ukiendelea kulinda ushindani wa soko na maslahi ya wakulima. Hivyo, Mwongozo huu umeandaliwa ili kusimamia ununuzi wa mazao kwa wasindikaji kupitia utaratibu wa aina mbili ambao ni **(i) Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na Minada ya Kidijitali na (ii) Mfumo wa Kutumia Vituo vya Kukusanyia Malighafi.** Utaratibu huu umewekwa kwa lengo la kuongeza usindikaji wa mazao, kukuza ajira na kuchochea ukuaji wa uchumi wa viwanda nchini.

*Jengo la Kahawa Plaza, Mtaa wa Njedengwa,S.L.P2780, Dodoma-Tanzania.*
*Simu:+255262310225, Baruapepe:info@copra.go.tz.*

**Aidha, mwongozo huu utafuata taratibu zote zilizopo katika mwongozo wa wakusanya mali wa mwaka 2026 na mwongozo mama wa biashara kwa mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde kwa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na Minada ya Kidigitali toleo namba tano (5) la mwaka 2026, isipokuwa majedwali ya mjengeko wa tozo namba 2,3,4 na 5 ambayo yamefanyiwa marekebisho katika mwongozo huu.**

## 2.0 MALENGO YA MWONGOZO

### 2.1 Lengo Kuu

Kuweka mfumo wa kitaifa wa usimamizi wa ununuzi wa nafaka na mazao mchanganyiko kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao nchini huku ukilinda maslahi ya wakulima na wadau wengine wa sekta.

### 2.2 Malengo Mahususi

Mwongozo huu unalenga:

i. Kuweka utaratibu wa kutambua na kusajili wasindikaji wanaostahili kununua mazao kupitia mfumo kwa utaratibu maalum;
ii. Kuweka vigezo vya wasindikaji watakaonufaika na utaratibu huu;
iii. Kuweka mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji wa matumizi ya mazao yanayonunuliwa kupitia mfumo;
iv. Kuhakikisha mazao yanayonunuliwa yanatumika kwa ajili ya uchakataji wa ndani na kuongeza thamani;
v. Kukuza uwekezaji katika viwanda vya kuongeza thamani ya mazao;
vi. Kukuza ajira kupitia shughuli za uchakataji wa mazao;
vii. Kuongeza ushindani wa bidhaa zilizoongezwa thamani katika soko la ndani na nje ya nchi;
viii. Kuongeza mapato ya Serikali kupitia biashara rasmi ya mazao na bidhaa zilizoongezwa thamani;
ix. Kuweka utaratibu wa utozwaji wa ada na tozo kwa wasindikaji;
x. Kuzuia matumizi mabaya ya mfumo wa wasindikaji kwa shughuli zisizolenga kuongeza thamani ya mazao nchini kwa kulinda mfumo rasmi wa biashara ya mazao;
xi. Uwazi wa bei na malipo kwa wakulima;
xii. Ufuatiliaji wa mwenendo wa malighafi kutoka kwa mkulima hadi kiwandani;

xiii. Kuongeza uwezo wa viwanda vya ndani kushindana katika soko;

xiv. Kuhakikisha usindikaji na biashara ya mazao inafanyika kwa kuzingatia taratibu za kitaifa.

## 3.0 MSINGI WA KISHERIA

Mwongozo huu umeandaliwa kwa mujibu wa:

- Sheria ya Usalama wa Chakula sura namba 249;
- Kanuni za biashara ya nafaka na mazao mchanganyiko ya mwaka 2015;
- Mwongozo wa biashara kwa mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawa na Kunde kwa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na Minada ya Kidigitali toleo namba tano (5) la mwaka 2026;
- Sheria nyingine zinazohusiana na biashara ya mazao, viwanda na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi.

## 4.0 TAFSIRI YA MANENO

Kwa madhumuni ya Mwongozo huu, isipokuwa kama muktadha utaeleza vinginevyo:-

**“COPRA”** maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko

**“Mfumo”** maana yake ni Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na Minada ya Kidijitali.

**“Msindikaji”** maana yake ni mtu, kampuni au taasisi inayojihusisha na uchakataji au kuongeza thamani ya nafaka na mazao mchanganyiko ndani ya Tanzania.

**“Bidhaa iliyoongezwa thamani”** maana yake ni bidhaa iliyochakatwa kutokana na mazao ghafi na kupata ubora, matumizi au thamani mpya ya kibiashara.

**“Mazao”** maana yake ni nafaka na mazao mchanganyiko yanayosimamiwa na COPRA.

**“Tozo”** maana yake ni ada, ushuru au gharama zinazotozwa katika mfumo wa biashara ya mazao.

**“Kiwanda”** maana yake ni eneo au mtambo unaotumika kwa ajili ya uchakataji wa mazao.

**“EPZA”** maana yake ni Export Processing Zones Authority.

**“TISEZA”** maana yake ni Tanzania Investment and Special Economic Zones Authority”.

## 5.0 ENEO LA MATUMIZI YA MWONGOZO

Mwongozo huu utatumika katika maeneo yote ya Tanzania Bara kwa wasindikaji wote wa nafaka na mazao mchanganyiko. Aidha, Mwongozo huu utahusu mazao yote yanayosimamiwa na COPRA na yatakayoruhusiwa kuuzwa kupitia mifumo rasmi wa biashara ya mazao.

Utaratibu huu umewekwa kwa madhumuni ya:

- Kurahisisha ufuatiliaji wa mtiririko wa malighafi kutoka kwa wakulima hadi kiwandani;
- Kuhakikisha vituo vya ukusanyaji vilivyosajiliwa vinafanya kazi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa;
- Kuwezesha COPRA kufuatilia taarifa za uzalishaji, ununuzi na hifadhi ya mazao kupitia mfumo wa COPRAMIS;
- Kuzuia mwingiliano usiodhibitiwa katika mifumo ya ununuzi wa mazao na kulinda uwazi wa biashara.

Mwongozo huu unaweka utaratibu wa aina mbili kwa wasindikaji watakaohitaji kununua mazao ili kusindika nchini.

i. Ununuzi kupitia vituo vya kukusanyia mazao vilivyosajiliwa
ii. Ununuzi kupitia mfumo wa stakabadhi za ghala na minada ya kidijitali

## 6.0 UTARATIBU WA UNUNUZI KUPITIA VITUO VYA KUKUSANYIA MAZAO

Huu ni utaratibu wa kununua mazao kupitia vituo vya kukusanyia mazao ambavyo vimesajiliwa na COPRA na kusimikwa mfumo wa kufuatilia hifadhi ya mazao. Katika vituo hivi mnunuzi atatakiwa kununua kwa bei isiyopungua asilimia 85 ya bei katika mnada na kutunza kila wakati kumbukumbu ya wakulima wanaomuuzia na bei anayonunulia. Msindikaji atakayehitaji kutumia mfumo huu, atawasilisha pia taarifa za kiwanda chake ambacho kitasajiliwa na kuwekewa mfumo wa ufuatiliaji wa hifadhi pia. Ufuatao ni utaratibu katika njia hii.

### 6.1 Uanzishaji wa Vituo vya Ukusanyaji

Msindikaji ataanzisha vituo maalumu vya kukusanyia malighafi katika mikoa atakayoruhusiwa kuendesha mfumo huu. Mikoa itatajwa katika barua ya idhini ya kuanza ununuzi.

Vituo hivi vitakuwa chini ya usimamizi wa msindikaji na vitatumika kwa ajili ya:

- Kupokea, kununua na kuhifadhi mazao kutoka kwa wakulima;
- Kukusanya na kuhifadhi taarifa za ununuzi kama zinavyohitajika katika mwongozo;
- Kufanya uhakiki wa ubora wa mazao kabla ya kusafirishwa kiwandani.

### 6.2 Usajili wa Vituo vya kukusanyia Mazao kama malighafi

Kabla ya kuanza kufanya kazi, kila kituo kitasajiliwa na COPRA na kutambuliwa kama **"Kituo Rasmi cha Ukusanyaji wa Malighafi"** kupitia mfumo wa COPRA MIS**.**

Ili kusajiliwa kituo kitakaguliwa iwapo kinakidhi vigezo vya kuhifadhi mazao kulingana na Kanuni za udhibiti Ubora wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko za mwaka 2026. Iwapo kituo kitakadhi vigezo, mmiliki au mwendeshaji atachukuliwa taarifa zake na kusajiliwa katika mfumo wa **COPRA MIS**. Mwendeshaji atahitajika kuwa anatunza taarifa za kiasi kinachonunuliwa na kuhifadhiwa katika kituo husika kupitia moduli ya kufatilia hifadhi ya mazao iliyo katika mfumo wa COPRA MIS.

### 6.3 Usajili na Utambuzi wa Wakulima

Msindikaji atatakiwa kutambua wakulima wote wanaouza mazao kupitia vituo vyake. Taarifa zitakazokusanywa ni pamoja na Jina la Mkulima, Eneo analotoka, Aina ya zao, Kiasi kilichouzwa, Bei aliyolipwa pamoja na namba ya simu ya mkulima. Taarifa hizi zitanakiriwa katika mfumo na mwendeshaji anapokuwa anapokea mazao.

### 6.4 Ukusanyaji na Ufuatiliaji wa Hifadhi ya Mazao ( Stock Moniroting)

Kiasi chote cha mazao kitakachokusanywa katika vituo vya msindikaji kitafuatiliwa kupitia mfumo wa **COPRAMIS**.

Mfumo utaonyesha:

- Taarifa za msingi za mkulima aliyeuza mazao;
- Kiasi kilichouza;
- Bei aliyouzia;
- Kiasi kilichoingia katika hifadhi ya kituo;
- Kiasi kilichotoka katika hifadhi ya kituo kuelekea kiwandani;

Vile vile Mazao yatakapofikishwa kiwandani kwa ajili ya usindikaji yataingizwa katika taarifa ya hifadhi ya kiwandani kupitia mfumo ambapo taarifa zifuatazo zitahifadhiwa.

- Kiasi cha mazao kinachopokelewa na kuhifadhiwa kiwandani;
- Kiasi cha mazao kilichosindikwa na kuondolewa kiwandani.

Lengo ni kuhakikisha ufuatiliaji wa mwenendo wa malighafi (stock movement) kutoka chanzo hadi bidhaa ya mwisho.

### 6.5 Utaratibu wa Malipo kwa Wakulima

Ili kuhakikisha ushindani na ulinzi wa wakulima, msindikaji atatakiwa kununua mazao kwa bei isiyopungua **Asilimia themanini na tano (85%) ya wastani wa bei iliyopatikana katika minada ya kidigitali.** COPRA itakuwa inatoa taarifa ya bei elekezi ya wastani kila wiki kupitia mfumo wa COPRAMIS.

### 6.6 Utoaji wa Kibali cha Usafirishaji wa Malighafi (Movement Permit)

Msindikaji atakapokuwa na mzigo wa kutosha kwa ajili ya kusafirisha kwenda kiwandani, atahitaji Kibali cha kusafirisha mzigo kitakachotolewa na COPRA baada ya kuwa na haya yafuatayo:

- Uthibitisho wa taarifa za hifadhi katika mfumo wa COPRA MIS kama ilivyoainishwa kwenye 6.4.
- Uthibitisho wa kiasi cha mzigo kinachohitajika kusafirishwa kwenda kiwandani;

Baada ya kuthibitisha uwepo wa taarifa hiyo, Mnunuzi atalipia tozo zinazohitajika kulingana na mwongozo huu na kisha kupatiwa kibali cha kusafirisha mazao **Movement Permit** ili kuyasafirisha kuelekea kiwandani.

Kibali hiki kitatumika kama miongoni mwa viambatisho pale msindikaji anapoomba kibali cha kusafirisha mazao yaliyosindikwa kwenda nje ya nchi.

## 7.0 UTARATIBU WA UNUNUZI WA MAZAO KUPITIA MFUMO RASMI WA MINADA YA KIDIGITALI

Ununuzi wa malighafi kupitia utaratibu huu utafuata masharti yafuatao;

i. Msindikaji aliyesajiliwa atanunua mazao kupitia mfumo rasmi wa minada ya kidijitali.
ii. Msindikaji atatambulika ndani ya mfumo kama “Msindikaji Aliyesajiliwa”.
iii. Mazao yatakayonunuliwa chini ya utaratibu huu yatatumika kwa ajili ya uchakataji ndani ya Tanzania pekee.
iv. Hairuhusiwi kuuza nje mazao ghafi yaliyonunuliwa chini ya utaratibu huu bila kibali cha COPRA.

v. COPRA inaweza kuweka ukomo wa kiasi cha mazao kitakachonunuliwa kulingana na:
    - Hali ya uzalishaji;
    - Mahitaji ya soko;
    - Uwezo wa uzalishaji wa kiwanda.

Taratibu zingine za ununuzi ni kama zilivyoanishwa katika Miongozo ya Biashara kwa mazao yanayosimamiwa na COPRA.

## 8.0 UTARATIBU WA UKAGUZI WA MAZAO KABLA YA KUSAFIRISHA NJE YA NCHI

Baada ya usindikaji kukamilika, na msindikaji kuhitaji kuandaa mazao kwa ajili ya kusafirishwa nje ya nchi, atahitajika kutoa taarifa COPRA ili kuhakiki kiasi kilichosindikwa kwa kulinganishwa na taarifa ya hifadhi ya mazao yaliyosindikwa iliyopo katika mfumo wa COPRA MIS.

Baada ya kukamilika kwa ukaguzi, kampuni itapewa **Kibali cha Kusafirisha Bidhaa Nje ya Nchi (Export Permit).**

### 8.4 Vigezo vya Msindikaji Anayestahili

Msindikaji atastahili kunufaika na utaratibu huu endapo atatimiza masharti yafuatayo:-

#### 8.4.1 Umiliki wa Kiwanda

Msindikaji awe na kiwanda halali kinachofanya kazi ndani ya Tanzania kwa ajili ya kuchakata zao husika.

#### 8.4.2 Usajili wa Kisheria

Awe amesajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania na awe na:

- Cheti cha usajili wa kampuni;
- Leseni ya biashara;
- Vibali vya uzalishaji vinavyotakiwa kisheria.

#### 8.4.3 Utambuzi wa Uwekezaji

Awe ametambulika au kusajiliwa na EPZA au mamlaka nyingine ya Serikali inayotambua wasindikaji au wawekezaji wa viwanda vya kuongeza thamani.

#### 8.4.4 Historia ya Uchakataji

Awe na ushahidi wa:

- Uchakataji wa mazao;
- Mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani;
- Usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi pale inapohitajika

#### 8.4.5 Uwezo wa Kununua Mazao

Awe na uwezo wa kununua kupitia mfumo kiasi kisichopungua **tani 10,000** kwa mwaka husika au kiwango kitakachopangwa na COPRA kulingana na hali ya uzalishaji na mahitaji ya soko.

#### 8.4.6 Mfumo wa Kumbukumbu

Awe na mfumo wa kutunza kumbukumbu za:

- Ununuzi wa malighafi;
- Uzalishaji;
- Mauzo;
- Usafirishaji wa bidhaa.

## 9.0 UTARATIBU WA USAJILI WA WASINDIKAJI

### 9.1 Maombi ya Usajili

Msindikaji atawasilisha maombi ya usajili kwa COPRA kwa kutumia fomu maalum.

### 9.2 Nyaraka za Kuambatisha

Maombi yataambatanishwa na:

i. Cheti cha usajili wa kampuni;
ii. Leseni ya biashara;
iii. Leseni au vibali vya uzalishaji;
iv. Ushahidi wa umiliki au uendeshaji wa kiwanda;
v. Taarifa ya uwezo wa uzalishaji wa kiwanda;
vi. Ushahidi wa mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani;
vii. Nyaraka nyingine zitakazohitajika na COPRA.

### 9.3 Tathmini ya Maombi

COPRA itafanya tathmini ya:

- Uhalali wa nyaraka;
- Uwezo wa uzalishaji;
- Uhalisia wa shughuli za uchakataji;
- Mahitaji halisi ya malighafi.

### 9.4 Utoaji wa Usajili

Baada ya kujiridhisha, COPRA itatoa cheti cha usajili wa msindikaji kitakachotumika ndani ya mfumo.

## 10.0 UKAGUZI WA VIWANDA

### 10.1 Ukaguzi wa Awali

COPRA itafanya ukaguzi wa kiwanda kabla ya kutoa usajili ili kuthibitisha:

- Uwepo wa kiwanda;
- Uwezo wa uzalishaji;
- Hali ya uzalishaji;
- Miundombinu ya uzalishaji;
- Mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu.

### 10.2 Ukaguzi wa Mara kwa Mara

COPRA inaweza kufanya:

- Ukaguzi wa kawaida;
- Ukaguzi wa kushtukiza;
- Ukaguzi wa uthibitisho wa matumizi ya malighafi.

### 10.3 Ushirikiano wa Msindikaji

Msindikaji atatakiwa:

- Kuruhusu ukaguzi;
- Kuwasilisha taarifa zinazohitajika;
- Kutoa nyaraka za uzalishaji na biashara.

## 11.0 MFUMO WA TOZO

**11.1 Utaratibu wa tozo kwa msindikaji atakayetumia mfumo wa vituo vya kukusanyia malighafi**

Kwa kila mzigo utakaonunuliwa kupitia mfumo huu, tozo zitakusanywa kama ifuatavyo:

| Na. | Taasisi | Tozo( Tsh/Kg) |
|---|---|---|
| 1 | Halmashauri | 02 |
| 2 | Mkoa | 02 |
| 3 | Maendeleo ya mazao | 30 |
| 4 | Maendeleo ya Ushirika | 40 |
| | **Jumla** | **74+3% CESS** |

**11.2 Utaratibu wa tozo kwa msindikaji atakayetumia mfumo wa stakabadhi za ghala na minada ya kidigitali**

**11.2.1 Punguzo la Tozo**

Msindikaji aliyesajiliwa atalipa asilimia 50 ya tozo zinazotozwa kwa wanunuzi wengine ndani ya mfumo. Kama inavyoonekana kwenye majedwali yanayofuata hapo chini yanavyoonesha.

**Jedwali namba 1:** Mjengeko wa Tozo kwa mazao ya Mikunde (Dengu, Mbaazi, Soya, Choroko, Njugumawe na Kunde);

| Na. | Aina ya Tozo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Gharama za Usimamizi za Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika | 30 |
| 2. | Mtunza Ghala | 18.5 |
| 3. | Ukaguzi | 1 |
| 4. | Dhamana ya Utunzaji Mazao Ghalani | 2 |
| 5. | Usafirishaji | 25 |
| 6. | Gharama za usimamizi wa mauzo | 2.5 |
| 7. | Usimamizi Mkoa | 1 |
| 8. | Usimamizi Wilaya | 1 |
| 9. | Vifungashio | 10 |
| 10. | Maendeleo ya zao | 15 |
| **Jumla ya Tozo** | | **106+ 3% CESS** |

**Jedwali namba 2:** Mjengeko wa Bei kwa zao la Ufuta;

| Na. | Aina ya Tozo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Gharama za Usimamizi za Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika | 50 |
| 2. | Mtunza Ghala | 18.5 |
| 3. | Ukaguzi | 1 |
| 4. | Dhamana ya Utunzaji Mazao Ghalani | 2 |
| 5. | Usafirishaji | 25 |
| 6. | Gharama za usimamizi wa mauzo | 2.5 |
| 7. | Usimamizi Mkoa | 1 |
| 8. | Usimamizi Wilaya | 1 |
| 9. | Vifungashio | 10 |
| 10. | Maendeleo ya zao | 15 |
| **Jumla ya Tozo** | | **126+ 3% CESS** |

**Jedwali namba 3:** Mjengeko wa Tozo baada ya msimu kufungwa ndani ya mkoa wa uzalishaji;

| Na. | Aina ya Tozo | Kiasi | |
|---|---|---|---|
| | | **Mikunde** | **Ufuta** |
| 1. | Maendeleo ya Ushirika | 21 | 23.5 |
| 2. | Maendeleo ya usimamizi stakabadhi za Ghala | 10 | 12.5 |
| 3. | Maendeleo za usimamizi wa mauzo | 10 | 12.5 |
| 4. | Usimamizi Mkoa | 15 | 20 |
| 5. | Usimamizi Wilaya | 25 | 30 |
| 6. | Maendeleo ya zao | 25 | 27.5 |
| **Jumla ya Tozo** | | **106+3%CESS** | **126+3%CESS** |

**Jedwali namba 4:** Mjengeko wa Tozo baada ya msimu kufungwa nje ya mkoa wa uzalishaji.

| Na. | Aina ya Tozo | Kiasi | |
|---|---|---|---|
| | | Mikunde | Ufuta |
| 1. | Maendeleo ya Ushirika | 50 | 50 |
| 2. | Maendeleo ya usimamizi stakabadhi za Ghala | 50 | 50 |
| 3. | Maendeleo za usimamizi wa mauzo | 50 | 50 |
| 4. | Maendeleo ya zao | 100 | 100 |
| **Jumla ya Tozo** | | **250** | **250** |

**Jedwali Na.5.** Mjengeko wa Tozo kwa mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, karanga na Choroko kwa wakusanya mali.

| Na. | Aina ya tozo | Mlipaji wa tozo kwa kila kilo | |
|---|---|---|---|
| | | Mkulima | Mnunuzi |
| 1. | Mtunza Ghala | 00 | 16.25 |
| 2. | Usimamizi wa mfumo wa stakabadhi za ghala | 00 | 03 |
| 3. | Kikosi kazi cha ukaguzi | 00 | 0.375 |
| 4. | Dhamana ya Utunzaji mazao Ghalani | 00 | 02 |
| 5. | Usafirishaji | 00 | 25 |
| 6. | Usimamizi wa mauzo | 00 | 05 |
| 7. | Usimamizi Mkoa | 00 | 01 |
| 8. | Usimamizi Wilaya | 00 | 01 |
| 9. | Vifungashio | 00 | 10 |
| 10. | Maendeleo ya zao | 00 | 15 |
| 11. | Ushuru wa Halmashauri | 00 | 1.5% |
| **Jumla ya tozo** | | | **78.625 + 3%** |

**NB:**

- *Tozo nyingine zote za maendeleo ngazi ya Mkoa na Halmashauri ambazo zipo nje na mwongozo huu, zitatolewa na wakulima kufuatia makubaliano yatakayofanyika na wana ushirika kupitia mikutano mikuu ya ushirika. Tozo hizi zitapitishwa kwenye mkutano wa wadau na kuidhinishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao mchanganyiko (COPRA);*
- *CESS itatozwa kwa kuzingatia Sheria.*

### 11.2.2 Madhumuni ya Punguzo

Punguzo hilo linalenga:

- Kuhamasisha uchakataji wa mazao ndani ya nchi;
- Kukuza viwanda vya ndani;
- Kuongeza ushindani wa bidhaa zilizoongezwa thamani.

### 11.2.3 Masharti ya Punguzo

Punguzo litatolewa endapo:

- Mazao yatatumika kwa ajili ya uchakataji;
- Msindikaji atazingatia masharti yote ya mwongozo.

## 12.0 HATUA ZA KIUDHIBITI

Endapo itabainika kuwa:

- Msindikaji ametumia mfumo vibaya;
- Mazao hayakuchakatwa kama ilivyokusudiwa;
- Kiasi cha bidhaa hakilingani na malighafi iliyonunuliwa;

COPRA inaweza kuchukua hatua zifuatazo:

i. Kumtaka msindikaji kulipa asilimia 100 ya tozo kwa kiasi chote kilichohusika;
ii. Kutoza adhabu kwa mujibu wa sheria;
iii. Kusimamisha usajili wa msindikaji;
iv. Kufuta usajili wa msindikaji;
v. Kuchukua hatua nyingine za kisheria.

## 14.0 WAJIBU WA COPRA

COPRA itakuwa na wajibu wa:

i. Kusimamia utekelezaji wa mwongozo huu;
ii. Kusajili wasindikaji;
iii. Kufanya ukaguzi na ufuatiliaji;
iv. Kusimamia mfumo wa taarifa ya hifadhi;
v. Kulinda maslahi ya wadau wa sekta;
vi. Kutoa elimu kwa wadau.

## 15.0 WAJIBU WA WASINDIKAJI

Wasindikaji watakuwa na wajibu wa:

i. Kuzingatia masharti ya mwongozo;
ii. Kutunza kumbukumbu sahihi;
iii. Kuwasilisha taarifa kwa wakati;
iv. Kuruhusu ukaguzi;
v. Kutumia mazao kwa uchakataji wa ndani.

## 16.0 MASHARTI YA JUMLA

i. COPRA inaweza kurekebisha mwongozo huu kadri itakavyoona inafaa.
ii. Mwongozo huu utasomwa pamoja na sheria nyingine za nchi.
iii. Pale ambapo kutakuwa na mgongano kati ya mwongozo huu na sheria za nchi, sheria za nchi zitazingatiwa.

## 17.0 HITIMISHO

Mwongozo huu umeandaliwa kwa lengo la kuhakikisha mfumo wa biashara ya nafaka na mazao mchanganyiko unaendelea kuwa rasmi, wenye uwazi na unaowanufaisha wadau wote wa sekta. Kupitia utekelezaji wake, Serikali inalenga kuongeza thamani ya mazao ndani ya nchi, kukuza viwanda vya ndani, kuongeza ajira, kuongeza mapato ya fedha za kigeni na kuchochea maendeleo ya uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Irene Mlola
**MKURUGENZI MKUU**